

African Union, African Regional Bodies

## Azimio kuhusu hali ya amani na usalama kwenye eneo la Sahara

Legislation as at 17 Oktoba 2019

There may have been updates since this file was created.

PDF created on 4 Oktoba 2024 at 10:02.

Tazama mtandaoni



Kuhusu mkusanyo huu

Sheria katika mkusanyo huu imetolewa tena kama ilivyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, na uumbizaji ulioboreshwa na makosa madogo ya uchapaji kusahihishwa. Marekebisho yote yametumiwa moja kwa moja kwenye maandishi na maelezo. Uchanganuzi wa gazeti asilia la kila kifungu cha sheria (pamoja na marekebisho) unapatikana kwa marejeleo.

[www.laws.africa](http://www.laws.africa)  
[info@laws.africa](mailto:info@laws.africa)

FRBR URI: /akn/aa-au/statement/resolution/pap/2019/5-3-7/swa@2019-10-17

There is no copyright on the legislative content of this document.

This PDF copy is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 License (CC BY 4.0). Share widely and freely.

African Union

## Azimio kuhusu hali ya amani na usalama kwenye eneo la Sahara

*Ilichapishwa mnamo 17 Oktoba 2019*

**Imeanza**

*[Hili ni toleo la hati hii kutoka 17 Oktoba 2019.]*

### **BUNGE LA AFRIKA,**

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika, ulioanzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha ushiriki kikamilifu wa watu wa Afrika katika maendeleo na utangamano wa kiuchumi wa bara;

**LIKIZINGATIA PIA** Ibara ya 3(a), (f) na (k) ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika inayoeleza malengo ya Umoja wa Afrika ili kuwa na umoja na mshikamano mkubwa miongoni mwa nchi za Afrika na watu wa Afrika, kukuza amani, usalama, na utulivu katika bara; kukuza ushirikiano katika nyanja zote za shughuli za binadamu ili kuboresha viwango vya maisha vya watu wa Afrika.

**LIKIZINGATIA ZAIDI** Ibara ya 3 ya Protokali ya Mkataba Anzilishi wa Jumuiya ya Uchumi ya Afrika inayohusiana na Bunge la Afrika, ambayo inawezesha utekelezaji kikamilifu wa sera na malengo ya Umoja wa Afrika; kukuza kanuni za haki za binadamu na demokrasia barani Afrika, na kukuza amani, usalama na utulivu.

**LIKIREJEA** Ibara ya 20 ya Mkataba Anzilishi ambayo pia inarejewa kwenye Ibara 9 ya Protokali ya Marekebisho ya Mkataba Anzilishi ya mwaka 2003; na Ibara ya 2 ya Protokali ya mwaka 2002 inayohusiana na Uanzishwaji wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kama "chombo kinachosimamia uamuzi wa kuzuia, kusimamia na kutatua migogoro.

**LIKIREJEA** Lengo la 4 la Ajenda 2063 ambalo linalenga kuwa na Muundo wa Amani na Usalama unaofanya kazi kikamilifu barani Afrika (APSA) kwa ajili ya kulinda amani, usalama na utulivu barani Afrika.

**LIKIZINGATIA** kwamba mabadiliko ya tabianchi ni moja ya changamoto kubwa zinazolikabili eneo la Sahara ambapo karibu asilimia 80 ya maeneo ya kilimo katika eneo la Sahara yameathirika na mabadiliko ya tabianchi hivyo kuathiri shughuli za kujiingizia kipato kwa watu wa eneo hilo;

**LIKITAMBUA KWA MASIKITIKO** kwamba kuongezeka kwa joto kwenye eneo la Sahara ni zaidi ya mara moja na nusu kuliko wastani wa dunia jambo ambalo limekuwa na athari kubwa kwenye upatikanji wa maji katika eneo la Sahara na kusababisha eneo hilo ambalo ni nusu jangwa kukabiliwa na changamoto kubwa za kudumu ikiwa ni pamoja na madhara makubwa ya mabadiliko ya tabianchi, mvua zisizotabirika, ukame wa mara kwa mara ambao umesababisha kupungua kwa mavuno na rasilimali ya maji kutokana na viwango vya juu vya joto katika eneo hilo ambavyo vinaathari mazingira;

**LIKITAMBUA pia KWA MASIKITIKO** kwamba ugaidi na siasa kali vinaendelea kuchochea kusambaa kwa silaha haramu ndogo ndogo ambazo zinatishia amani na usalama barani Afrika na kukwamisha juhudi za kuboresha hali za maisha ya watu wa Afrika;

**LIKITAMBUA PIA** kwamba sababu tofauti zinachangia uhamiaji haramu, usafirishaji haramu wa binadamu na mashambulizi ya kigaidi ya mara kwa mara yanayofanywa na AQIM na Boko Haram na makundi mengine ya kigaidi katika eneo la Sahara;

**LIKITAMBUA ZAIDI** kiwango cha silaha ndogo ndogo zinazosambaa katika eneo la Sahara; na madhara yake kwa amani na usalama kutokana na kuzuka kwa mapigano ya mara kwa mara, vitendo vya kigaidi na siasa kali barani;

**LIKIRIDHISHWA** na juhudi zinazofanywa na serikali kwenye eneo la SAHARA na jukumu linalotekelezwa na Baraza la Amani na Usalama katika Kanda hiyo;

**KWA MUJIBU WA** ya Kanuni 5 (b), (c) na (d) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo pamoja na mambo mengine, inalipa BA madaraka ya kuandaa mijadala, kujadili, kutoa maoni, kutoa mapendekezo kuhusiana na malengo na jambo lolote linalohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vyake, Jumuiya za Uchumi za Kanda, Nchi Wanachama na vyombo na taasisi zake;

**SASA LINAAZIMIA:**

Kuunda tume ya kutafuta ukweli wa mambo kwenda eneo la SAHARA ili kutathmini wakimbizi na hali ya kibinadamu kwenye eneo hilo na athari zake kwa amani, usalama na utulivu kwenye eneo hilo.

**Limepitishwa Midrand, Afrika Kusini**

**17 Oktoba 2019**